

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA TATU

02 FEBRUARI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA TATU – TAREHE 02 FEBRUARI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

37. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa Ikungi.

38. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakasimu kwa TANROADS barabara ya Kibaoni, Kakunyu hadi Bugango wakati taratibu za kupandisha hadhi zikiendelea.

39. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini adha ya Walimu kukaa chini kwa kukosa Ofisi Shule za Msingi Maendeleo, Bonyokwa, na Kinyerezi Jica itatatuliwa.

40. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko, Stendi, Dampo, Machinjio na barabara kwa Km 12 za lami kupitia TACTIC katika Mji wa Mbulu.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

41. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru Wananchi wa Manispaa ya Mtwara dhidi ya vumbi la makaa ya mawe.

42. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni kwa kiasi gani Taasisi za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinashirikiana katika shughuli za kiuchumi.

WIZARA YA NISHATI:

43. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama ya gesi ili kuepuka matumizi ya mkaa na kuni.

WIZARA YA MAJI:

44. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini maji yatasambazwa Toangoma, Chamazi, Mianzini, Kilungule, Kiburugwa, Kijichi, Mbagala, Charambe, Kibondemaji na Mbagala Kuu.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

45. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu majengo yaliyopo maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

46. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaboresha jengo la Kituo cha Polisi Konde, Wilaya ya Micheweni.

WIZARA YA KILIMO:

47. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itafanya Kilimo kuwa Kipaumbele cha kwanza cha Taifa kwa kupunguza bei ya mbolea.

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**DODOMA
02 FEBRUARI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

